**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**KIKAO CHA KWANZA**

**28 JANUARI, 2020**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 28 JANUARI, 2020

**I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:**

**II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA TATU ASUBUHI:**

**III. TAARIFA YA SPIKA:**

**IV. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.8) wa Mwaka 2019 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019]*.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.8) wa Mwaka 2019 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019]*.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.8) wa Mwaka 2019 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019]*.

**V. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**1. MHESHIMIWA LIVINGSTONE JOSEPH LUSINDE (MTERA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini barabara ya Mvumi *Mission* itajengwa kwa kiwango cha lami.

2. **MHESHIMIWA RUTH HIYOB MOLLEL (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Shule ya Msingi Vikindu katika Wilaya ya Mkuranga ina mikondo miwili (A na B) Darasa la Kwanza hadi la Saba, na mwaka 2019 Darasa la Kwanza na la Pili lilikuwa na Wanafunzi 300 kila Darasa:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha uwiano wa Mwalimu na Mwanafunzi wa 1:45 unazingatiwa kwa mujibu wa Sera ya Elimu ya Msingi;

(b) Je, kwa msongamano huo tunaweza kupata Wanafunzi walioelimika na kukidhi malengo ya Tanzania ya viwanda.

3. **MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Ipo ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara yenye urefu wa Kilomita nane inayopita katikati ya Mji wa Itigi:-

Je, ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa.

## WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**4. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu ya malimbikizo ya madeni mbalimbali ya Wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali ikiwemo huduma ya kupeleka chakula kwa Wafungwa Magerezani na matengenezo ya magari:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulipa madeni hayo.

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**5. MHESHIMIWA MOHAMED OMARY MCHENGERWA (RUFIJI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Wilaya ya Rufiji ni moja ya Wilaya kongwe nchini na inakadiriwa kuwa na watu takribani 350,000; eneo la Wilaya ni kubwa na huwalazimu Wananchi kusafiri umbali wa km 100 kufuata huduma za kibenki:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma za kibenki katika Wilaya ya Rufiji.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**6. MHESHIMIWA DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF (MGOGONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Kutokana na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kumekuwa na ongezeko kubwa la makosa katika Jamii, jambo ambalo linasababisha mfumo wa utoaji haki pamoja na Mahakama kuelemewa:-

(a) Je, kila Jaji au Hakimu anapangiwa kesi ngapi kwa mwaka ili kupunguza mlundikano wa kesi;

(b) Je, ni mambo gani kimsingi yanayosababisha mashauri kuchukua muda mrefu.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**7. MHESHIMIWA KHADIJA HASSAN ABOUD (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Idara ya uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's) inafanya kazi zake kwa weledi na uadilifu mkubwa lakini haina mamlaka ya kujitegemea kama zilivyo BRELA na RITA:-

Je, ni lini Serikali itaipa mamlaka Idara hiyo kuwa Taasisi inayojitegemea.

**8. MHESHIMIWA SIKUDHANI YASINI CHIKAMBO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Kumekuwa na wimbi kubwa la Watoto wa mtaani ambao wanaishi katika mazingira magumu:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia Watoto hao.

**9. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mashine mpya ya *X – Ray* katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara – Ligula.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**10. MHESHIMIWA DKT. SAADA SALUM MKUYA (WELEZO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni nini kinasababisha baadhi ya bidhaa zinazozalishwa Zanzibar kupata vikwazo kuingia katika Soko la Tanzania Bara.

**WIZARA YA MAJI:**

**11. MHESHIMIWA JOSEPH ROMAN SELASINI (ROMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Jimbo la Rombo hususani Ukanda wa chini wenye takribani Vijiji 41 lina shida ya maji; na Halmashauri imeanzisha mradi wa kupanua bomba kubwa la maji linalotoka Marangu. Aidha, Halmashauri ilipendekeza vyanzo vingine ikiwemo matumizi ya maji ya Ziwa Chala, uchimbaji wa visima na mabwawa yatokanayo na mito ya msimu:-

(a) Je, Serikali imekubali mpango wa kuanza kutumia maji ya Ziwa Chala;

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kutosha ili mradi huo uweze kuanza.

**12. MHESHIMIWA FELISTER ALOYCE BURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Kutokana na Serikali kuhamia Dodoma, mahitaji ya maji safi na salama yamekuwa makubwa na

kwa sasa mgao wa maji kwa Wakazi wa Dodoma umeshaanza:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuhakikisha Wakazi wa Dodoma wanapata maji safi na salama.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**13. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Serikali iliahidi katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kujenga malambo, majosho na kisima kirefu kwa ajili ya Wananchi wafugaji wa Kata ya Ruvu Jimbo la Same Magharibi:-

Je, ni lini ahadi hiyo itakamilishwa.

**VI. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020 *(The Arbitration Bill, 2020).*

## VII. SHUGHULI YA KUKABIDHI MAJOHO KWA MASPIKA WASTAAFU:

1. Mhe. Anne Semamba Makinda;

2. Mke wa Marehemu Mhe. Samuel John Sitta (Mhe. Margaret Simwanza Sitta);

3. Mheshimiwa Pius Chipanda Msekwa.

## VIII. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.8) wa Mwaka 2019 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.8) Bill, 2019]*.

**DODOMA**
**28 JANUARI, 2020**

**S. KAGAIGAI**
**KATIBU WA BUNGE**